

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

BUNGE LA TANZANIA



ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

MKUTANO WA SABA

KIKAO CHA TATU

08 APRILI, 2022



ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

MKUTANO WA SABA

KIKAO CHA TATU – TAREHE 08 APRILI, 2022

I. DUA

II. MASWALI:

OFISI YA RAIS (TAMISEMI):

21. ● **MHESHIMIWA MRISHO MASHAKA GAMBO (ARUSHA MJINI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):-

Je, Jiji la Arusha lina Wamachinga wangapi, wapo maeneo gani na wangapi wamepatiwa vitambulisho kufikia Mwezi Februari, 2022.

22. **MHESHIMIWA AYSHAROSE NDOGHOLI MATTEMBE (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):-

Je, ni lini Serikali itapeleka gari la kubebea Wagonjwa katika Hospitali ya Wilaya ya Mkalama.

WIZARA YA MALIASILI NA UTALII:

23. MHESHIMIWA LUHAGA JOELSON MPINA (KISESA):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maliasili na Utalii:-

Je, ni lini Serikali itarejesha kwa Wafugaji mifugo iliyokamatwa na TAWA, TFS na WMA ambapo Mahakama ilitoa hukumu irejeshwe.



WIZARA YA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WANAWAKE NA MAKUNDI MAALUM:

24. MHESHIMIWA NUSRAT SHAABAN HANJE (VITI MAALUM):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum:-

Je, Serikali ina mkakati gani wa kuzuia ukatili wa kijinsia na utumikishaji wa Watoto kwenye Kambi tarajiwa za Mradi wa Bomba la Mafuta Hoima.

WIZARA YA FEDHA NA MIPANGO:

25. MHESHIMIWA DKT. FAUSTINE ENGELBERT NDUGULILE (KIGAMBONI):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Mipango:-

Je, ni lini Serikali itapitia gharama za leseni kwa Wabunifu wa *Apps* za huduma za kifedha na kuwawezesha kutumia mifumo iliyopo.

26. MHESHIMIWA KHADIJA SHAABAN TAYA (VITI MAALUM):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Mipango:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kuhakikisha Sensa ya Watu na Makazi inajumuisha takwimu za Watu wenye Ulemavu na aina ya ulemavu.

WIZARA YA MAMBO YA NDANI YA NCHI:

27. MHESHIMIWA NDAISABA GEORGE RUHORO (NGARA):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi:-

Je, ni lini Serikali itakamilisha ujenzi wa Vituo vya Polisi vya Nyamagana, Keza na Djululigwa vilivyojengwa na Wananchi.

28. MHESHIMIWA MOHAMMED SAID ISSA (KONDE):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kufanya ukarabati wa Kituo cha Polisi cha Konde katika Wilaya ya Micheweni.



WIZARA YA UJENZI NA UCHUKUZI:

29. MHESHIMIWA SUMA IKENDA FYANDOMO (VITI MAALUM):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi:-

Je, ni lini Serikali itaanza ujenzi wa Barabara ya Igawa hadi Tunduma kwa kiwango cha lami.

**WIZARA YA HABARI, MAWASILIANO NA
TEKNOLOJIA YA HABARI:**

**30. MHESHIMIWA CONDESTER MICHAEL
SICHALWE (MOMBA):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Habari,
Mawasiliano na Teknolojia ya Habari:-

Je, ni lini Serikali itatatua Migogoro ya Mikatiba
ya Minara ya Simu kati ya Kampuni za Simu na
Kijiji cha Namuchinka Kata ya Kapele.

III. HOJA ZA SERIKALI:

WAZIRI MKUU:

Kwamba, Bunge sasa likubali kupokea na kupitisha
Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Waziri
Mkuu kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023.

(Majadiliano yanaendelea)

**DODOMA
08 APRILI, 2022**

**N.J. MWIHAMBI, *ndc*
KATIBU WA BUNGE**